

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MUHTASARI WA MPANGO WA USHIRIKISHAJI WADAU (STAKEHOLDERS ENGAGEMENT PLAN - SEP)

WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA TANZANIA YA KIDIJITALI (DTP)

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unajumuisha mchakato wa kushirikisha wadau kwa lengo la kufikia malengo yaliyokubalika. Kwa sasa imetambulika kuwa utaratibu wa uwajibikaji ni wa kimsingi kwani unalazimisha Taasisi kushirikisha wadau katika kutambua na kuelewa mpango/mradi maalum na hivyo kutoa majibu ya maswala na hoja mbalimbali zinazotolewa na wadau kwa ajili ya maamuzi au utekelezaji na hivyo kuboresha utendaji wa programu / mradi .

DTP inakusudia kuongeza upatikanaji wa huduma bora za mtandao kwa serikali na raia na kuboresha uwezo wa serikali wa kutoa huduma za umma za kidijitali.

Programu ya Tanzania ya Kidigitali ina vipengele vitano (5):

- ✓ Kipengele cha Kwanza: Ekolojia ya Kidijitali.
- ✓ Kipengele cha Pili: Miundombinu ya uunganishaji wa Kidijitali.
- ✓ Kipengele cha Tatu: Jukwaa la Huduma za Kidijitali
- ✓ Kipengele cha nne: Usimamizi wa Mradi
- ✓ Kipengele cha tano: Kukabiliana na Dharura.

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) huu utasimamiwa na kutekelezwa na Timu ya Mazingira na Jamii ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH), Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) na Kitengo cha Utekelezaji wa Miradi (PIU). Lengo kuu la SEP hii ni kufafanua mchakato wa ushiriki wa wadau wa DTP, utoaji wa habari kwa umma na mashauriano. Aidha, SEP hii inaelezea njia ambazo wasimamizi wakuu wa mradi wa DTP (yaani WMTH, OR-MUUUB na PIU), washauri na wakandarasi watakavyokuwa wanawasiliana na wadau, utaratibu ambao watu wanaweza kuelezea hoja zao, jinsi hoja zilizoibuliwa zitakavyoshughulikiwa na kujibiwa.

Wadau hawa waliotambuliwa ni wale wanaoathiriwa na / au wahusika wanaopenda kufuatilia na wawakilishi rasmi na wasiyo rasmi. Utambuzi wa wadau chini kwenye mradi wa DTP utategemea (i) kazi na majukumu yao; na uwezekano wa ushawishi wao / wanaopenda kufuatilia mradi. Umakini utawekwa hasa kwa wale walio katika hatari ya kutengwa na shughuli za miradi ya DTP.

Wadau watakaoshirikishwa kwenye Mradi wa DTP ni pamoja na:

- ✓ Waathiriwa Chanya - kikundi cha watu au mashirika yanayoguswa na shughuli za mradi au jamii.
- ✓ Waathiriwa Hasi - ni pamoja na watu binafsi na taasisi zilizo na masilahi katika ardhi ambayo itapitiwa na shughuli ya mradi. Wengi wa hawa ni wamiliki wa ardhi walio na majengo au mashamba ambayo yataathiriwa na upotevu wa ardhi, majengo na mapato ya kiuchumi.
- ✓ Vikundi vingine - kikundi cha watu au mashirika yanayopenda kufuatilia shughuli mbali mbali ikijumuisha watetezi wa mradi, serikali za mitaa au ya kitaifa
- ✓ Mamlaka, wanasiasa wa ndani au wa kitaifa, mamlaka za jadi, viongozi wa dini, asasi za kiraia pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali
- ✓ Watu walio katika mazingira hatarishi wanaotambuliwa ambao ni pamoja na, watoto, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee na vijana.

Utoaji wa habari na mashauriano na wadau utafanywa kupitia njia na mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na majadiliano ya vikundi (kulingana na umri, jinsia na kazi), mahojiano, watoa habari muhimu na barua pepe. Ushauri utafanywa kwa wakati muafaka kwa washiriki kulingana na maoni yao na pia kutumia lugha yao ya kienyeji.

Maoni kutoka kwa wadau yatapokelewa na wasimamizi wa utekelezaji wa mradi wa DTP katika fomu zilizojazwa kupitia maandishi na zilizojazwa baada ya mahojiano kwa mdomo (kwa kutumia visanduku vya maoni, viongozi wa mitaa, mikutano ya hadhara, mahojiano n.k.). Timu itakagua maoni ya wadau na kurejesha maazimio ya mwisho na muhtasari wa jinsi maoni yalivyozingatiwa.

Ili kushughulikia malalamiko yanayohusiana na mradi wa DTP kutoka kwa jamii na umma zilizoathirika, na utaratibu rasmi wa kupokea tathmini na kushughulikiwa, utaratibu wa uwazi wa Ushughulikiaji wa Malalamiko (GRM) kwa mradi DTP utaandaliwa. Kutaanzishwa Kamati za Ushughulikiaji wa Malalamiko katika wanufaika wa Mradi / na vile vile katika Kitengo cha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mradi wa DTP (PIU). Kwa wafanyakazi walioajiriwa na wakandarasi, wakandarasi watatakiwa kutoa utaratibu wao wa Ushughulikiaji wa Malalamiko kama sharti la zabuni ambayo kwa kiwango cha chini inazingatia mahitaji haya.

Hati hii ya SEP inaweka mkakati na mpango wa utekelezaji kwa wadau wanaohusika kuanzia mwanzo wa mradi hadi kukamilika kwake.

Hata hivyo SEP ni uti wa mgongo wa mradi kuweza kufanikiwa kikamilifu na kwa ufanisi. Ni hati ya moja kwa moja ambayo itakuwa inapitiwa na kuhuishwa pale itakapolazimu, kila mwaka kuonyesha mabadiliko katika ushiriki wa wadau kulingana na maendeleo ya mradi na wadau wapya kama wapo.